TANGAZO LA SERIKALI NA. 383 la tarehe 15/5/2020

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA. 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA PUMBA ZA MAZAO YA NAFAKA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME YA MWAKA 2020

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Jina la sheria

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Pumba za Mazao ya Nafaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2020.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote lililo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Same.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo-

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Same;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri au afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kutekeleza kazi za Mkurugenzi;

"mkulima" maana yake ni mtu anayejishughulisha na kilimo ili kukidhi mahitaji yake ya kila siku;

"mfanyabiashara" maana yake ni mtu anayejishughulisha na uuzaji wa bidhaa za viwandani na mazao ya mashambani ;

"ushuru''maana yake ni ushuru unaotozwa na Halmashauri kwa shughuli za ununuzi wa pumba katika eneo la Halmashauri ;

"pumba" maana yake ni mabaki yanayopatikana baada ya mazao ya nafaka kukobolewa;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au taasisi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri.

SEHEMU YA PILI :
USHURU WA PUMBA

Ushuru wa pumba

**4**. (1) Kutakuwa na ushuru wa pumba utakaolipwa na mnunuzi wa pumba.

(2) Kiwango cha ushuru kitakuwa ni Shilingi Elfu Moja kwa kila gunia lenye uzito wa kilogramu mia moja.

(3) Ushuru wa pumba utakusanywa na Halmashauri au wakala kwa kadri itakavyoelezwa.

(4) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumzuia mtu kununua au kusafirisha pumba endapo itabaini kuna ukiukaji wa Sheria Ndogo hii.

Uwezo wa afisa mwidhiniwa

**5**. Afisa Mwidhiniwa wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii atakuwa na uwezo katika muda wa kazi, muda wa ununuzi au

usafirishaji wa pumba-

(a) kuingia katika jengo lolote kwa lengo la kukusanya ushuru ; na

(b) kukagua eneo au chombo chochote atakachokitilia mashaka kuwa kinahifadhi au kusafirisha pumba au kinatumika kukwepa kulipa ushuru.

SEHEMU YA TATU
MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu

**6**. (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) amekwepa kulipa ushuru chini ya Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa ushuru bila uhalali wowote wa kisheria;

(c) kwa makusudi atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri;

(d) atamzuia afisa mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake.

(2) Mtu akitiwa hatiaoni kwa kosa lolote chni ya kifugu kidogo cha (1) atapewa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kufililisha kosa

**7.** Mkurugenzi anaweza kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yoyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria

Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hii na kuwa tayari kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Kufutwa Tangazo Na. 564/2015

**8.** Sheria Ndogo hii iinafuta Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Pumba za Mazao ya Nafaka) ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2015

______

JEDWALI

______

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 8)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi…………………………………….nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya…………………………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya SAME kwamba tarehe……ya Mwezi……………..Mwaka ………….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ………………………cha Sheria Ndogo ya Ushuru wa Pumba za mazao ya Nafaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2020.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri nipo tayari kulipa kiasi cha shilingi laki mbili na kutimiza wajibu wangu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hiyo badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO NILIYOTOA HAPO JUU NI KWA HIARI YANGU NA KWA KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo Tarehe…………………ya Mwezi…………………Mwaka………………………..
Jina…………………………………..
Saini………………………………….

Mbele ya:
Jina………………………………………..
Cheo………………………………………
Saini………………………………………

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Same umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa Azimio lililopitishwa na mkutano wa baraza la Madiwani ulioitishwa tarehe 15/3/2018.

ANNA CLAIRE SHIJA
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Same*

CHRISTOPHER M. IRIRA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,Same*

NAKUBALI,

L.S

*Dodoma,*
16 Aprili, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*WN OR-TAMISEMI*
*Dodoma*